

Je! mabalasi Bwana Yesu aliyoyatumia kugeuzia maji kuwa divai,  
yalitumika tu kwa kazi hiyo?

**SWALI:** Shalom Wapendwa Samahani Nilikuwa Nauliza Katika Kitabu Cha Yohana 2:1 Na Kuendelea Katika Harusi Ya Kana Yesu alitumia “MABALASI” ile Mitungi Ya Kujitawadhia kugeuza maji kuwa Divai, swali linakuja je? ilikuwa ni kawaida kutumia hiyo mitungi kuwekea divai au kulikuwa na vyombo vingine.

---

**JIBU:** Mabalasi vilikuwa ni vyombo maalumu vya kuhifadhia vitu...Ni kama leo tuseme mapipa!..unaweza kwenda mahali ukakuta nyumba moja pipa wanalitumia kuwekea maji ya kunywa, pengine wanawekea mbegu za mazao, mahali pengine wanatumia pipa kuhifadhia pombe wanazotengeneza, sehemu nyingine wanatumia kuwekea maji ya kwenda bafuni n.k Na hapo katika habari hiyo, Mabalasi ni kama mapipa, isipokuwa hapo yalitumika kwa kutawadhia. Na kutawadha kunakozungumziwa hapo, sio kule kwa chooni, bali ni kule mtu anapojisafisha sehemu baadhi za mwili kama mikono na miguu...kabla ya kuingia kwenye Ibada, hiyo ilikuwa ni desturi za Wayahudi,...Na ilikuwa mtu hajisafishi ndani ya hilo balasi, hapana! Bali anachota maji kutoka kwenye hilo balasi na kujisafisha kando...

kama Bwana Yesu alivyowatawadha wanafunzi wake miguu kabla ya kushiriki meza ya Bwana (*soma Yohana 13:1-18*)...Hivyo mabalasi hayo

Je! mabalasi Bwana Yesu aliyoatumia kugeuzia maji kuwa divai,  
yalitumika tu kwa kazi hiyo?

ya kutawadhia vilikuwa ni vyombo visafi na si vichafu. Na kwanini  
Bwana Yesu aliagiza yatumike hayo Mabalasi na si vyombo vingine?...Ni  
kwasababu ndio vyombo pekee viliyyokuwa karibu na pale alipo  
(maeneo yale) na vilikuwa tupu

*Yohana 2:6 "Basi kulikuwako huko mabalasi sita ya mawe, nayo  
yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha, kila  
moja lapata kadiri ya nzio mbili tatu.*

*7 Yesu akawaambia, Jalizeni mabalasi maji. Nao wakayajaliza hata  
juu".*

Ni kama tulivyosema, pipa hilo hilo linaweza kutumika kuhifadhia  
pombe, na pipa hilo hilo linaweza kutumika kuhifadhia maji, au mazao  
au taka, n.k.... Hivyo kama biblia inavyotuambia hapo mabalasi hayo  
yalitumika kwa ajili ya kutawadhia...lakini Bwana Yesu alilyaona  
yanaweza kufaa pia kwa kuwekea divai, ndipo akageuza maji yale kuwa  
divai ndani ya mabalasi yale, na watu walikunywa bila kuona shida  
yoyote wala kinyaa..kwasababu pengine ilishazoeleka na ilikuwa  
inajulikana kuwa mabalasi pia yanatumikaga kwa shughuli za kuhifadhia  
Divai ..

Je! mabalasi Bwana Yesu aliyoyatumia kugeuzia maji kuwa divai,  
yalitumika tu kwa kazi hiyo?

Ubarikiwe!

---

**Mada Nyinginezo:**

**MATUMIZI YA DIVAI.**

**JE! ULEVI NI DHAMBI?**

**MTEGEMEE MUNGU, NA SI MWANADAMU.**

**NJAA ILIYOPO SASA.**

**UNALITUMIA KWA HALALI NENO LA KWELI?.**

**MSTARI HUU UNA MAANA GANI? “TUPA CHAKULA CHAKO  
USONI PA MAJI; MAANA UTAKIONA BAADA YA SIKU NYINGI”.**

**(MHUBIRI 11:1)**

---

Je! mabalasi Bwana Yesu aliyoyatumia kugeuzia maji kuwa divai,  
yalitumika tu kwa kazi hiyo?

## **Rudi Nyumbani:**

Share on:

WhatsApp